

TAARIFA YA KATA YA IWIFI

UTANGULIZI

Kata ya Iwiji inapatikana ndani ya Mkoa wa Mbeya Wilaya ya Mbeya katika ukanda wa chini wa milima ya Umalila, upande wa mashariki inapakana na Wilaya ya Ilenje, na Magharibi inapakana na Wilaya ya Mbozi, Kusini Mbeya Vijijini ambazo ni kata za Isuto, Illembu na kwa upande wa kasikazini inapatikana na Kata ya Itale ambayo ipo Wilaya ya Ileje mkoa wa Songwe.

Kata ya Iwiji inajumla ya Vijiji vitatu ambayo ni Kijiji cha Iwiji, Isende na Izumbwe II ambapo Vijiji hivi vinajumla ya vitongoji 26 kama vinavyooneshwa hapa chiniambavyo vinaunda Kata hii ya Iwiji. Ifuatayo ni orodha ya Vitongoji kama inayonekana kwenye jedwali hapa chini; -

JINA LA KATA	JINA LA KIJINI	MAJINA YA VITONGOJI
IWIFI	IWIFI	Iwiji, Ipasa, Mabula, Tambalale, Soweto, Ntinga, Magowe, Mtukula na Vimetu
	ISENDE	Isende, Masala, Nachingungwe, Klashi, Shihola, Shinandala na Luma
	IZUMBWE II	Shilanzi, Hayende, Ileya A, Ileya, Chawama, Sayuma, Kafule, Ikese, Rupamba na Songwe

Asili ya watu

Kata ya Iwiji inayo jumla ya makabila matatu ambayo ni Wamalila, Wandali pamoja na Wanyiha.

Viongozi ngazi ya Kata ni kama ifuatavyo

Kata ya Iwiji inaongozwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata (KAMAKA) ambapo mwenyekiti wa kamati hiyo ni diwani na katibu wake ni mtedaji wa kata (WEO)

1. Diwani ni Mhe. shimiwa Thomas Michael Kibona
2. WEO ni Speratus C. Bamuhiga

Ikama ya watumishi

Kata ya Iwiji inajumla ya watumishi 57 ambao ni kama ifuatavyo; -

Na.	IDARA	CHEO	IDADI	JUMLA
1	UTAWALA	WEO	1	4
		VEO	3	
2	ELIMU	MSINGI	27	44
		SEKONDARI	17	
3	KILIMO NA MIFUGO	WAEO	1	3
		VAEO	2	
4	AFYA	MGANGA	2	6
		NESI	4	
JUMLA KUU				57

Vyanzo vya mapato

Kata ya Iwiji vyanzo vyake vya mapato ni Kilimo cha msimu, Pamoja na gulio ambalo linafanyika kila Jumamosi ya juma, Kijiji cha Iwiji ndipo gulio linapatikana.

Shughuli za kiuchumi

Shughuli za kiuchumi zinazoendeshwa katika kata ya Iwiji ni uzalishaji wa kilimo pamoja na mifugo, kama inavyooneshwa kwenye majedwali hapo chini:

Wastani wa Uzalishaji wa Kilimo cha Chakula kwa Mwaka

MAZAO YA CHAKULA	Ha.	TANI
MAHINDI	1199.1	2098.4
MAHARAGE	468.55	253.01
VIAZI MVIRINGO	89.2	42.82
VIAZI VITAMU	37	3.35
NGANO	19.3	0.67
MIGOMBA	313.7	3537.6
MBOGA MBOGA	18.6	112.5
MAPARACHICHI	13.5	1518.7
JUMLA	2158.95	7,567.05

Wastani wa Uzalishaji wa Mazao ya Biashara kwa Mwaka

MAZAO YA BIASHARA	Ha.	TANI
KAHAWA	1057.7	22159.4
PARETO	9.7	9.7
JUMLA	1,067.4	22,169.1

Wastani wa Uzalishaji wa Mifugo kwa Mwaka

Na.	AINA YA MFUGO	IDADI
1	Ng'ombe wa asili	1565
2	Ng'ombe wa maziwa	87
3	Mbuzi wa asili	1313
4	Mbuzi wa kisasa	8
5	Nguruwe	223
6	Kuku wa asili	2731
7	Kuku wa kisasa	1954
8	Kondoo	125
9	Mbwa	157
10	Sungura	417
11	Simbilisi	220
	JUMLA	8800

Huduma za kijamii

Kata ya Iwiji ina jumla ya Shule za msingi tano (5) ambazo ni Shule ya msingi Iwiji, Isende, Sayuma, Izumbwe II na Shihola Kata ya Iwiji ina Shule moja ya Sekondari ambayo ni Iwiji.

Kata ya Iwiji ina jumla ya vituo vya zahanati viwiili (2) ambavyo ni Zahanati ya Kijiji cha Iwiji, Pamoja na Zahanati ya Kijiji cha Izumbwe II.

Kata ya Iwiji inao mradi wa maji unaohudumia Kijiji cha Iwiji kwa Vitongoji baadhi ambavyo ni Iwiji, Mabula, Ipasa na Vimetu. Chanzo cha mradi huu wa maji ni Kijiji cha Iwala Kata ya Itale Wilaya ya Ileje Mkoa wa Songwe.

Kata ya Iwiji inayo machinjio moja ambayo ni nguvu kazi ya Wananchi (yaani ilijengwa na Wananchi wa Kijiji cha Iwiji). Machinjio hii ni ya Ng'ombe ,Mbuzi , Kondoo na Nguruwe

Kata ya Liweji inajumla ya maghala mawili ambayo yanapatikana katika Vijiji vya Iiwji pamoja na KIjiji cha Isende, maghala haya yanasaidia Wakulima na Kata hii kuhifadhi mazao hasa msimu wa kilimo hasa kilimo cha Mahindi na Kahawa.

Kata ya Iwiji inajumla ya vikundi arobaini na moja (41) ambapo vikundi 3 ni vya Wanawake, 3 nivya vijana , 3 ni vya Waviv, 31 ni vikundi mchanganyiko pamoja na kikundi 1 cha kikoba.

Kata ya Iwiji inayo miradi mbalimbali ambayo inaendelea na shughuli za Ujenzi katika Vijiji tofauti tofauti vinavyounda Kata hii, Miradi hiyo ni kama ifuatavyo; -

1. Ujenzi wa vyoo Wanafunzi Shule ya msingi Iwiji ambayo imefikia usawa wa lenta
2. Ujenzi wa vyoo Shule ya msingi Isende Kijiji cha Isende, ambapo vyoo viro katika hali ya mashimo
3. Ukarabati wa vyumba vya madarasa Shule ya msingi Shihola Kijiji cha Isebde
4. Ujenzi wa vyoo Vyumba za Walimu Shule ya msingi Izumbwe II
5. Ujenzi wa choo Shule ya msingi Izumbwe II amba ujenzi upo hatua ya shimo
6. Ujenzi wa vyumba ya Mwalimu Shule ya msingi Sayuma Kijiji cha Izumbwe II ambapo ujenzi upo hatua ya upauaji pamoja na ujenzi wa choo cha Wanafunzi ambapo kipo katika hatua za kupaua lakini bado uchimbaji wa Shimo
7. Ujenzi wa Shule, Ujenzi huu unafanywa na vitongoji vitatu(3) kutoka Kijiji cha Iwiji(yaani Tambalale, Soneto na Mtukula). Ujenzi huu ulianza mwaka 2008 ambapo mpaka sasa kuna vyumba(2) madarasa, Ofisi za Walimu, vyoo vya Wanafunzi matundu 10, vyoo vya Walimu, vyumba ya Mwalimu ambayo hatua za umalizaji.
8. Ujenzi wa Zahanati ya Kijiji cha Isende ambayo ipo katika hatua ya upauaji ambapo pia mahitaji muhimu yote yapo
9. Ujenzi wa jengo la ofisi ya Kijiji cha Iwiji, Ujenzi huu unaendelea ambapo mpaka sasa umefikia katika hatua ya lenta